MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
DAWASA
Dar es Salaam Water Supply & Sanitation Authority
ISO 9001:2015 Certified

DAWASA YETU

TAREHE: 22 SEPTEMBA - 28 SEPTEMBA 2024 | TOLEO NA. 0176

# DAWASA MTAA KWA MTAA YAHITIMISHWA KWA KISHINDO KINONDONI

## Zaidi ya Wateja 3000 waboreshewa huduma za Maji Goba na Wazo



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (**DAWASA)** imehitimisha kwa kishindo kampeni ya DAWASA mtaa kwa mtaa katika kata za **Goba na Wazo** wilaya ya Kinondoni ambapo wateja zaidi ya **3000** wamefikiwa na kuhudumiwa.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha kampeni hiyo kwa naiba ya Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu **Ndugu Paul Sulley** ameeleza kuwa kupitia kampeni hiyo wateja **3000** wa kata za **Goba** na **Wazo** wamefikiwa na kutatuliwa changamoto za kihuduma ambazo ni pamoja na kurejeshewa huduma kwa wateja waliositishiwa kutokana na madeni kwa kuwapa mikataba ya kulipa kidogo kidogo na kufanikiwa kuunganishwa huduma ya maji kwa wateja wapya waliokamilisha taratibu za kupata huduma.

"Zoezi hii limerudisha tabasamu kwa wakazi wa **Goba** na Wazo, zoezi lilifanyika siku tatu kuanzia **Septemba 19-21** na lilianza kwa kuweka Dawati la huduma na leo limehitimishwa kwa Watumishi wa ofisi kuu za Mamlaka wa Mwananyamala na Ubungo kupita nyumba kwa nyumba kuhudumia Wananchi." alisema Sulley.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa huduma kwa wateja **CPA (T) Ritamary Lwabulinda** ameeleza kuwa zoezi hilo ni endelevu na limesaidia kuwafikia wateja na kuwasikiliza kwa dhumuni la kuboresha huduma.

"Tumepata ushirikiano mkubwa kwa wateja wetu wametueleza changamoto mbalimbali ikiwemo ikiwemo wizi wa mita unaoendelea katika maeneo yao na sisi tumewapa elimu ya jinsi ya kuzilinda kwa kuzijengea kisasa ili zisiweze kuibiwa" aliongezea **Rithamary Lwabulinda**

**Gwanta Mwalopo** mkazi wa mtaa wa **Mivumoni** amesema ujio wa **DAWASA** ni neema kwao ambapo wameweza kutatuliwa changamoto zao.

"Ujio wa **DAWASA** leo na vifaa vyao tumeona wameziba mivujo iliyokuwa inaharibu barabara zetu lakini pia wametupa mawasiliano yao ikitokea changamoto nyingine tuweze kuwasiliana nao" alisema **Bi. Mwalopo**

Zoezi la **DAWASA** mtaa kwa mtaa ni endelevu lenye lengo la kuwafikia wananchi katika maeneo yao ili kuwasikiliza na kujenga mahusiano bora katika wananchi na Mamlaka.

DAWASA MOJA, NGUVU MOJA, KAZI IENDELEE